
www.ippmedia.com

# Alasiri Online

**Alhamisi Januari 31, 2019** Tanzani 500/- Kenya 50/-




# YA JAY DEE, GADNER YARINDIMA

## KUMBE NAY ANAJUA MAHABA

# YA JAY DEE, GADNER YARINDIMA

Na Mary Kadoke

UZALENDO umemshinda aliyekuwa mume wa muimbaji Jay Dee, Gadner G Habash baada ya kukiri kuwa pamoja na kuachana kwao, hakuwahi msahau mtalaka wake.

Msimamo huo unakuja baada ya kuzua gumzo katika mtandao wa Instagram kupitia ukurasa wake @ captaintanzania aliporusha picha akiwa amemkumbatia Jay Dee.

Tafsiri ya mtu anayekumbukwa ni mtu uliyemsahau, hivyo kuchuliwa kwamba amemkumbuka aliyekuwa asali wake kwa picha si sawa kwani amekuwa kweye akili yake siku zote amezungumza hayo alipofanya mahojiano na Alasiri Online.

"Sijawahi kumsahau Lady Jaydee, naomba nieleweke, nimesema na nitaendelea kusema ndiyo maana mtu akiniuliza kama nimemkumbuka namshangaa kwa sababu mtu anayekumbukwa ni yule aliyesahaulika," amesema.

"Kwangu Jay Dee sijamsahau hata kidogo, yupo tu siku zote kwenye akili yangu," amesisitiza Gadner.

Jitihada za kumsaka Jay Dee ili kujua msimamo wake juu ya hizi salamu hazikuzaa matunda kwani simu yake iliishia kuita bila kupokelewa.

Kupitia akaunti ya @captaintanzania alirusha picha akiwa na mtalaka wake Jaydee walioishi miaka 15 kabla ya kuachana 2016 na kuipa 'caption', "Throwing it back (TBT) na Songster @jidejaydee Nairobi katika kisima Awards.

Picha hiyo ilizua gumzo kutoka kwa mashabiki baadhi wakihoji kama wamerudiana huku wengine wakiwapongeza kumaliza tofauti zao.

"Jamani nimeipenda hiyo nimekumbuka mbali sana" aliandika Happymasisi.

Hii couple nilikuwa naipenda sana natamani siku moja nisikie tena mko pamoja," aliandika oliverbenson.

"Mmm kwani kuna habari gani?" alihoji kiba_fan.



# Kibona: Injili inalipa



Na Anaeli Mbise

MSANII wa muziki wa Injili Ipyana Kibona amesema miaka 15 ya utumishi wa kiroho umemlipa kuliko angebaki katika taaluma ya utabibu.

Akizungumza na Alasiri Online, muimbaji huyo wa kibao 'Moyo Wangu' amesema anakuwa na furaha kuimba Injili kwa sababu anawatibu watu wengi kiroho, kimwili na kiafya.

"Sijutii kuacha kazi yangu ya udaktari, kwa kutumia nyimbo zangu nawafikia watu wengi sana na huko nawatibu kiroho, kimwili na kiafya jambo ambalo linanipa faraja na kunitia nguvu," amesema Kibona.

Aidha, ameongeza kuwa muziki wa Injili kwa siku za hivi karibuni umekua kibiashara kutokana na matamasha mengi kuingizia wasanii kipato.

"Maisha hayana formula siku za nyuma mtu alikuwa anakaa kwenye fani yake, lakini miaka hii nimeona mambo yanabadilika unapiga kazi tofauti na uliyosomea cha msingi unaangalia kipato unachoingiza tu," amesema Kibona.



# MZIWANDA: MUZIKI KWANZA, NDOA BAADAYE

Na Anaeli Mbise

NUH Mziwanda ambaye kwa sasa anaishi kisela baada ya kuachana na mkewe, amesema hana mpango wa kuoa kwa sasa.

Akizungumza na Alasiri Online, mwanamuziki huyo wa kizazi kipya amesema kuwa anaweka nguvu nyingi katika muziki kwa mwaka 2019, ili azidi kupaa zaidi kitaifa na kimataifa na mambo ya mahusiano ya ndoa hayapi tena nafasi.

"Ninasema bado nipo nipo kwanza hadi hapo baadaye nitakapoona kuna haja ya kuvuta jiko, lakini kwa sasa ni bora niendelee kuwa peke yangu," amesema Mziwanda.

Msanii huyo ambaye sasa anashuti video ya wimbo wa Natapatapa, amesema ameamua kuupa nafasi kubwa muziki akiamini kwamba bado ni kijana mdogo na pia ataoa wakati ukifika.

## KUMBE NAY ANAJUA MAHABA

Na Mary Kadoke

MFOKAJI Nay wa Mitego kutoka tasnia ya Bongo Fleva amekuja na jiwe lingine, 'Mbele kwa mbele' baada ya kutamba na ngoma ya Hakuna Maisha magumu.

Asilimia kubwa ya maudhui yaliyomo kwenye ngoma hiyo ni umaridadi wake anaotumia kama silaha ya kumridhisha mpenzi wake wakiwa katika uwanja wao wa mapenzi.

Akizungumza na Alasiri Online Nay ameeleza kuwa nia ya kuachia ngoma hiyo ni kuwashawishi wanaume kuzidisha ubunifu kwa wapenzi wao hasa wanapokuwa faragha.

"Si kila siku nitaimba politics au kutoa maoni kuhusu kazi au uchumi ndio maana awamu hii nikaamua kuja kivingine kidogo," amesema.

"Si vibaya kumsifia mpenzi wako, tunaimba politics, uchumi, kazi sometimes sio mbaya kumsifia mpenzi wako hasa yale mambo yetu," aliongeza Ney.

Tangu kuachiwa kwa ngoma hii iliyo katika mfumo wa sauti na video una wasikilizaji 316,000 mpaka sasa katika mtandao wa YouTube.

Ney kupitia ngoma yake ya awali, Hakuna Maisha magumu alilenga zaidi kuhamasisha vijana kutochagua kazi kwani kupitia kazi hizo huchangia kukuza vipato vyao na taifa kwa ujumla.



# HABARI KITAIFA



## Billnass aleza kisa cha kutumia watoto

Na Anaeli Mbise

MWANAMUZIKI Billnass amefunguka sababu za kuwatumia watoto wadogo katika 'video' ya ngoma mpya.

Akizungumza na Alasiri Online, Billnass amesema kuwa maamuzi hayo ni kwa ajili ya kuweka kitu cha kitofauti katika video hiyo.

"Sababu ya kuamua kuwatumia wale watoto ni kufanya kitu cha tofauti, badala ya kutumia kila siku video vixen tukaamua kufanya vile, lakini pia Bilnass wazo lake lilikuwa ni kuwa baba na mimi pia niwe baba mwingine," amesema Billnass.

Pia Billnass amezungumzia jinsi walivyofanya nao kazi na amesema ilikuwa rahisi kutokana na vipaji ambavyo vinaonekana kama wanajua kuigiza.

"Mai ni mbaya sana, yaani kila ukimwelekeza kitu anafanya hapo hapo, tofauti na Chonge alikuwa anamsikiliza director kile anachoambiwa anafanya," amesema Billnass.

## Jamani Ndauka anataka mtoto



Na Anaeli Mbise

NYOTA wa Bongo movies Rose Ndauka amesema bado ana ndoto ya kupata mtoto wa pili kama akipata mwanamume sahihi.

Akizungumza na Alasiri Online, Ndauka amesema anajisikia raha anapokuwa na mtoto wa kwanza, lakini anadhani ni wakati umefika wa kuongeza mwingine.

"Ninataka kuongeza mtoto wa pili, lakini tatizo ni mwanamume wa kuzaa naye sijampata, ila ninaamini Mungu ni mwema atanipa mtu sahihi wa kuzaa naye," amesema Ndauka.

Ndauka amecheza filamu za Bongo kama vile Angela, Sitaki Tena na Bad Girl na sasa anajihusisha na masuala ya kukuza vipaji ambayo ina lengo ya kunyanyua vipaji na kuvikuza katika tasnia ya filamu.